# ELCT/KARAGWE DIOCESE

Telegram-EVANGEL
Telephone No. 255-28-2223334
Fax No: 255-28-2223284
E-mail: main-nyakahanga@kad.or.tz
doctor-nyakahanga@kad.or.tz
Web: www.karagwe-diocese.or.tz
www.nyakahangahospital.org

NYAKAHANGA
DESIGNATED DISTRICT HOSPITAL
P.O. BOX 110, KARAGWE Via BUKOBA
TANZANIA East Africa


Kumb. Na.NH/A.74/677 14/03/2023

## TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mganga Mkuu wa Hospitali Teule ya Wilaya Karagwe – Nyakahanga, kupitia kibali cha ajira Mbadala kilichotolewa na Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, chenye Kumb. Na.FA.10/128/01"M"/75 kilichotolewa tarehe 27/02/2023, anawatangazia wananchi wote wenye sifa za kuajiriwa katika kada zifuatazo:-

### 1. AFISA MUUGUZI MSAIDIZI DARAJA LA II (ANO) – Nafasi mbili (2)

**A: Sifa za mwombaji**
- Awe na elimu ya Kidato cha nne
- Awe na Stashahada (Diploma) ya Uuguzi kutoka chuo kinachotambuliwa na Serikali
- Awe amesajiliwa na baraza la Wauguzi na wakunga Tanzania
- Awe na leseni hai

**B: Kazi na majukumu**
- Kutoa huduma za uuguzi
- Kukusanya takwimu muhimu za afya
- Kuwaelekeza kazi wauguzi walio chini yake
- Kuelimisha wagonjwa na jamii kuhusu matatizo yao ya kiafya
- Kutoa huduma za kinga na uzazi
- Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi zinazohusiana na elimu, uzoefu na ujuzi wake.

**C: Mshahara**
Ngazi ya Mshahara itaanzia TGHS B.I

### 2. Mteknolojia (Mionzi) II – Nafasi moja (1)

**A. Sifa za Mwombaji**
- Mhitimu mwenye kidato cha nne/Sita
- Mwenye stashahada ya Mionzi kutoka chuo kinachotambuliwa na Serikali
- Awe amesajiliwa na baraza pale inapohusika

**B. Kazi na Majukumu**
- Kupima wagonjwa wanaoelekezwa kwenye eneo lake la kazi
- Kutunza mitambo na vifaa vya radiolojia katika eneo lake la kazi
- Kukagua picha za x-ray zilizopimwa kwa ubora na kutosheleza(diagnostic quality)
- Kutunza picha za wagonjwa hadi majibu yanapowafikia madaktari waliowatuma wagonjwa
- Kusimamia watumishi walio chini yake
- Kutoa ushauri kuhusu masuala ya kazi za radiolojia na mionzi katika eneo lake la kazi
- Kuandaa vifaa vya tiba/uchunguzi na kusimamia utakasaji vifaa katika eneo lake la kazi
- Kutoa mafunzo ya awali kwa watumishi wanaopangiwa kazi katika eneo lake la kazi
- Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi zinazohusiana na elimu, uzoefu na ujuzi wake.

**C. Mshahara.**
- Nganzi ya mshahara itaanzia TGHS B.I kwa mwezi.

**3. NURSE II (Muuguzi Daraja la II) – Nafasi mbili (2)**

**A. Sifa za mwombaji**
- Awe amehitimu na kupata cheti baada ya kozi ya miaka miwili toka chuo kinachotambuliwa na serikali.
- Awe na leseni hai

**B. Kazi na majukumu**
- Kuhudumia wateja katika eneo atakalopangiwa kutumika
- Kusimamia na kuratibu kazi za wahudumu wa afya katika sehemu yake ya kazi
- Kukusanya takwimu na kutayarisha taarifa za utendaji wa kazi
- Kutoa ushauri nasaha
- Kutoa huduma za kinga na uzazi wa mpango
- Kuelimisha wagonjwa na jamii kuhusu matatizo ya kiafya na jinsi ya kujikinga na magonjwa mbalimbali
- Kutunza vifaa na vitendea kazi vilivyo katika maeneo yake ya kazi
- Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu mkuu wako wa kazi zinazohusiana na elimu, uzoefu na ujuzi wako

**C. Mshahara**
- Nganzi ya mshahara itaanzia TGHS A.I kwa mwezi.

**4. Mteknolojia (Dawa) II – Nafasi moja (1)**

**A. Sifa za mwombaji**
- Awe amehitimu kidato cha nne/sita mwenye stashahada ya famasi kutoka chuo kinachotambuliwa na Serikali.
- Awe amehitimu mafunzo ya vitendo kazini(internship) ya mwaka mmoja
- Awe amesajiliwa na Baraza la Famasi
- Awe na leseni hai

**B. Kazi na majukumu**

- Kuainisha mahitaji ya mwaka ya dawa na vifaa na kuandaa bajeti yake
- Kuagiza,kununua, kuhifadhi na kusambaza dawa na vifaa tiba hospitalini
- Kuweka kumbukumbu za dawa
- Kuandaa orodha ya dawa za hospitali(Hospitali fomulary) kwa hospitali
- Kutoa dawa na vifaa tiba kwa wagonjwa
- Kusimamia matumizi sahihi ya dawa
- Kutengeneza dawa(compounding) kwa matumizi ya kituo anapofanya kazi
- Kutoa taarifa juu ya madhara yatokanayo na matumizi ya dawa(adverse drug reaction)
- Kuwa katibu wa Kamati za tiba ya Hospitali(Hospital Therapeutic Commitee)
- Kuelimisha watumshi walio chini yako, watumishi wengine wa sekta ya afya na jamii juu ya matumizi sahihi ya dawa.
- Kusimamia utekelezaji wa Sera ya Taifa ya dawa hospitalini
- Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi zinahusiana na elimu, uzoefu na ujuzi wake.

C. Mshahara

- Nganzi ya mshahara itaanzia TGHS B.I kwa mwezi.

**MASHARTI YA KUAJIRIWA KWA WAOMBAJI WOTE**

- Awe ni raia wa Tanzania
- Awe na umri kuanzia miaka 18 hadi 45
- Awe hajawahi kupatikana na kosa lolote la jinai, kufungwa jela, au kufukuzwa katika utumishi wa umma
- Mwombaji aambatishe maelezo binafsi (CV), vyeti vya taaluma, vyeti vya kidato cha nne na cha sita, cheti cha kuzaliwa, **cheti cha NIDA** na picha mbili (2) za rangi (passport size) za hivi karibuni.
- Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na kuhidhinishwa na mamlaka husika (TCU na NACTE) na taarifa ya uhakiki iambatishwe kwenye maombi.
- Uwakilishaji wa taarifa na sifa za kughushi wahusika watachukuliwa hatua za kisheria
- Barua zote ziandikwe kwa mkono
- Mwisho wa kutuma maombi haya ni tarehe 30/03/2022, saa 10.00 jioni.

Maombi yote yatumwe kwa anwani ifuatayo:-

**Mganga Mkuu**
**Hospitali ya Nyakahanga**
**S.L.P 110**
**Karagwe.**

Tangazo hili limetolewa na,

Mchg. Sevelin S. Malozi
**K.n.y Mganga Mkuu**

K.n.y. MGANGA MKUU
HOSPITALI YA NYAKAHANGA

**Nakala**

1. Katibu Mkuu – KKKT DKAR, S.L.P 7, Karagwe
2. Mkurugenzi Mtendaji – Halmashauri ya Wilaya Karagwe, S.L.P 20 Karagwe